

WARAKA WA PILI WA YOHANA KWA WATU WOTE

¹ Mimi Mzee nakuandikia wewe Bimkubwa mteule, pamoja na watoto wako ninaowapenda kweli. Wala si mimi tu ninayewapenda, bali pia wote wanaoujua ule ukweli wanawapenda ninyi, ² kwa sababu ukweli unakaa nasi milele. ³ Neema na huruma na amani zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Yesu Kristo, Mwana wa Baba, zitakuwa pamoja nasi katika ukweli na upendo. ⁴ Nilifurahi sana kuona kwamba baadhi ya watoto wako wanaishi katika ukweli kama Baba alivyotuamuru. ⁵ Basi, Bimkubwa, ninalo ombi moja kwako: tupendane. Ombi hili si amri mpya, bali ni amri ileile tuliyokuwa nayo tangu mwanzo. ⁶ Upendo maana yake ni kuishi kwa kuzitii amri zake Mungu. Amri niliyoisikia tangu mwanzo ndiyo hii: mnapaswa nyote kuishi katika upendo. ⁷ Wadanganyifu wengi wamezuka duniani, watu ambao hawakiri kwamba Yesu Kristo amekuja kwetu akawa binadamu. Mtu asemaye hivyo ni mdanganyifu na ni Adui wa Kristo. ⁸ Basi, jihadharini ninyi wenyewe ili msije mkapoteza kile mlichokishugulikia, bali mpate tuzo lenu kamili. ⁹ Asiyezingatia na kudumu katika mafundisho ya Kristo, bali anayakiuka, hana Mungu. Lakini anayedumu katika mafundisho hayo anaye Baba na Mwana. ¹⁰ Basi, kama mtu akija kwenu bila kuwaleteeni mafundisho hayo, msimkaribishe

nyumbani kwenu, wala msimsalimu. ¹¹ Maana anayemsalimu mtu huyo, anashirikiana naye katika matendo yake maovu. ¹² Ninayo mengi ya kuwaambieni lakini sipendi kufanya hivyo kwa karatasi na wino; badala yake, natumaini kuwa-tembeleeni na kuzungumza nanyi ana kwa ana, ili furaha yetu ikamilike. ¹³ Watoto wa dada yako mteule wanakusalimu.

Biblia Takatifu
Portions of the New Testament in the Swahili
Language of Kenya, Mozambique, Somalia, and
Tanzania, translation by Dr. Johann Ludvig Krapf
completed in 1850

Public Domain

Language: Kiswahili (Swahili)

Dialect: Kimvita

Translation by: Dr. Johann Ludvig Krapf

2014-08-25

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 22 Feb 2024 from source files
dated 31 Aug 2023

62071dc0-70e6-5b86-b569-c1b45e7771bd